**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE**

**Mambo muhimu ya kuzingatia kwa anayejiunga na Shule ya Sekondari Kasansa.**

**A. SARE YA SHULE**

**I. WASICHANA**

**DARASANI**

- Sketi mbili (02) za rangi ya udongo. Inatakiwa iwe na urefu unaofika kwenye kifundo cha mguu (kisigino), Mshono wa sketi ni Rinda box iwe na mfuko mmoja kulia na zipu na huksi upande wa kushoto. Ukishona sketi za kubana utarudishwa na ni marufuku mwanafunzi kuvaa sketi ya kubana na mtindo mwingine usioelekezwa.
- Fulana yenye rangi ya damu ya mzeena nembo ya shule.
- Shati nyeupe jozi mbili yenye mikono mifupi na isiyo na urembo wowote. Wanafunzi wa kiislamu washone nusu kanzu nyeupe itakayoambatana na hijabu yake.
- Tai yenye rangi ya udongo
- Jozi mbili za Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi na vyenye kamba.
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Sweta moja rangi ya damu ya mzee

**KAZINI**

- Gauni moja yenye rangi ya kijani yenye mshono wa solo ndefu inayofika kwenye kisigino.

**MICHEZO**

- Traksuti ya rangi ya bluu nyeusi (Dark blue)
- Raba nyeupe

**II. WAVULANA**

**DARASANI**

- Suruali mbili (02) za rangi ya udongo inatakiwa iwe inchi 21 kwenye mkunjo wa chini (turn up), isiyo bana makalio, mifuko miwili mbele (siyo kama jinsi) na mfuko mmoja kulia nyuma na iwe na rinda mbili mbele. Ukishona modo utarudishwa na ni marufuku mwanafunzi kuvaa modo na mtindo mwingine usioelekezwa.
- Fulana yenye rangi ya damu yam zee na nembo ya shule.
- Shati nyeupe jozi mbili yenye mikono mifupi na isiyo na urembo wowote. Wanafunzi wa kiislamu washone nusu kanzu nyeupe itakayoambatana na hijabu yake.
- Tai yenye rangi ya udongo

